# Wingi wa kodi unavyoua utalii Tanzania




Watalii wa nje wakivinjari katika moja ya mbuga za wanyama nchini. Pamoja na Sekta ya Utalii kuwa muhimu kwa uchumi wa Taifa, wadau wake wanalalamikia utitiri wa kodi kuwa unahatarisha mustakabali wa sekta hiyo. Picha ndogo ni moja ya vivutio vya utalii vilivyopo nchini. **Picha ya Maktaba**

**Adam Ihucha**, Mwananchi
aihucha@mwananchi.co.tz

Peter Lesongoyo, aliposimama mbele ya waandishi wa habari, wengi katika mkusanyiko huo walitaka kudondosha machozi kutokana na simulizi yake aliyoitoa kwa unyonge.

Kijana huyu wa jamii ya Wamaasai mwenye umri wa miaka 28, kutoka kijiji cha Engaresero Kaskazini mwa Tanzania, anaonekana mwenye huzuni kutokana na watalii kuacha kutembelea katika jamii yake.

Yeye hufanya kazi ya kuonyesha utamaduni wa Kimasai ambao ni kivutio kwa watalii na hivyo kujipatia riziki.

Hata hivyo, watalii hawajatembelea tena jamii hiyo kwa hivi karibuni, hali inayotishia maisha yake na wenzake wanaotegemea kazi hiyo kujiingizia vipato.

"Sijui itakuwaje iwapo watalii hawataingia mpaka wiki ijayo. Labda wengine tutakufa njaa," anaeleza huku akionyesha wasiwasi kwamba labda utamaduni wao siyo kivutio tena kwa wageni.

Alexis Cronin, mtalii kutoka Ulaya, anaeleza kwa nini watalii wanashindwa kutembelea vivutio vingi mara kwa mara. "Wingi wa kodi katika maeneo tunayotembelea ni changamoto sana," anasema.

Wakati mnufaika huyo wa utalii na mtalii akilalamika kuhusu kodi, wafanyabiashara wa sekta hiyo nao wanalalamikia hali hiyo kuwa inawafanya washindwe kufanya biashara ya utalii kwa ufanisi.

Kodi hizo na masharti mengine ya kiudhibiti siyo tu ni vingi bali vinakusanywa na mamlaka tofauti zilizopo sehemu tofauti na hivyo kugharimu fedha na muda wa kulipia.

Kwa wastani, mfanyabiashara wa utalii ikijumuisha wenye hoteli, anatumia takriban saa 2,000 kwa mwaka kutekeleza masharti ya leseni, kulipa kodi na masharti mengine. Hii ni kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Dk Hawa Eve Sinare kwa ajili ya Chama cha wenye hoteli nchini.

Utafiti huo unasema, kinachokwamisha kukua kwa utalii wa Tanzania ni mambo mengi ikiwamo masharti kwa wawekezaji wa ndani na nje ikilinganishwa na sekta nyingine za uchumi.

Kodi nyingi, leseni nyingi, pamoja na gharama kubwa za uendeshaji hufanya mazingira yawe magumu zaidi, kwa mujibu wa utafiti huo.

Taarifa hiyo inatoa mfano wa mambo yanavyokuwa magumu wakati mwingine kutokana na mpangilio wa matukio tu. Kwa mfano, mwekezaji wa utalii anatakiwa awe amenunua magari yake yote kwa jina la kampuni yake na yawe yameingizwa nchini kabla hajapewa leseni.

Ili mwekezaji apate cheti cha kupata motisha kutoka kituo cha uwekezaji ambacho kitampa unafuu wa kodi za kuingiza bidhaa ikiwamo magari ni lazima awe na leseni ya kufanya biashara ya utalii.

Ili mwekezaji huyu pia afungue akaunti ya benki kwa jina kampuni yake, ni lazima awe amepata leseni baada ya kukabidhiwa cheti cha motisha kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Ripoti hiyo inasema Sekta ya Utalii ina udhibiti na usajili unaojirudia rudia bila sababu kutoka mamlaka za usimamizi nchini.

Wafanyabiashara wa utalii wanadaiwa kodi zipatazo 32 , huku 12 zikiwa za usajili na leseni.

Wadau wa sekta hii ya utalii wanasema kodi hizo ndizo zinaifanya Tanzania ionekane kama nchi ghali kwa watalii wa nje.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Utalii, Willy Chambullo anasema kinachoumiza zaidi ni namna ya ulipaji na muda unatumika kutekeleza masharti hayo. "Kwa hapa Tanzania, ni rahisi kulipa faini kwa kufanya biashara kinyume cha sheria kuliko kutekeleza masharti ya ufanyaji biashara hasa kodi," anasema.

"Inabidi kuziangalia kodi katika sekta ya utalii na kuzipunguza kama tunataka kweli kupata watalii 2,000.000 ifikapo mwaka 2017 kama inavyotajwa na kushindana na nchi nyingine zenye vivutio kama vya kwetu." anasema mkurungenzi mtendaji wa chama cha wenye hoteli nchini, Lathifa Sykes.

Hofu kubwa ya wadau hawa wa utalii ni kwamba huenda watalii wa Tanzania wakaenda zaidi Kenya, kwani nchi hiyo inayopakana na Tanzania kwa upande wa Kaskazini inafanya mikakati mingi kuboresha utalii wake uliovurugwa na mambo ya kiusalama.

Tanzania ina kampuni zipatazo 1,050 za biashara ya utalii, lakini ni 300 tu zinazotekeleza masharti ya kulipa kodi kutokana na ugumu uliopo wa mifumo ya ulipaji kodi.



## DOKEZO

**Tanzania ina kampuni zipatazo 1,050 zinajishughulisha na biashara ya utalii lakini ni 300 tu zinazotekeleza masharti ya kulipa kodi kutokana na ugumu uliopo wa mifumo ya ulipaji kodi**

## SAUTI ZA WATU

### Furaha Nsemwa

**Nchi yetu inabidi ilifufue tena Shirika la ndege la ATCL ili lisafiri ndani na nje ya nchi. Hiyo italeta ushindani utakaopelekea kushuka kwa nauli za ndege na hivyo kuwafanya watalii waje kwa wingi. Ndege hii inabidi pia ianzishe safari kwenda kwenye maeneo yenye vivutio vya utalii. Kwa upande wa kodi kwa watalii na wafanya biashara ya utalii, serikali izipitie upya na kutengeneza mazingira yatakayowawezesha wafanyabiashara kuzilipa kwa wakati mmoja. Wizara ya Utalii inabidi iwaone watalii wote ni sawa badala ya kutegemea wazungu tu.**

### Elineema Saro

**Ili kuboresha mazingira ya sekta binafsi yafuatayo yafanyike; kwanza mfumo wa elimu ubadilike ili wahitimu waandaliwe kujiajiri na kuwa wajasiriamali badala ya kuwa wasakaji ajira. Pili serikali izidishe upendeleo kwa wasambazaji, makandarasi, watoa huduma na washauri wa Kitanzania badala ya wageni. Tatu Serikali iongeze ujenzi wa miundombinu ya kijamii na kiuchumi ili kuiweka nchi kwenye nafasi ya kuwa sehemu ambayo uzalishaji ni wa gharama ndogo ma. Serikali ipunguze urasimu kwenye huduma kama leseni, vibali na kodi.**

UKURASA HUU UMEDHAMINIWA NA
BEST-Dialogue
Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo